# SERA YA JINSIA KATIKA VYOMBO VYA HABARI

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

# SERA YA JINSIA KATIKA VYOMBO VYA HABARI

© Baraza la Habari Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2020

Toleo la Pili 2021

ISBN: 978-710-85-0

# SERA YA JINSIA KATIKA VYOMBO VYA HABARI



Tuhesabu-Kuna wanawake wangapi katika picha hii?

## UFAFANUZI WA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

**Ubaguzi:** Hii ni hali yoyote ya kumtendea jambo mtu au kutomtendea, kumtenga ama kumfanyia jambo kwa namna ya kipekee ambayo inamnyima ama kumpunguzia hadhi yake moja kwa moja au kwa namna nyingine kwa misingi ya jinsia yake, utaifa, ujauzito, umri, ulemavu, nchi atokayo, ndoa au vigezo vingine kama hivyo.

**Vyombo vya Habari:** ni nyenzo zote za kuwezesha uwepo wa mawasiliano, ikiwa ni pamoja na mikondo yote ya upashanaji habari ikijumuisha ile ya kizamani na ile ya zama hizi ya kidijitali.

**Maadili ya Uanahabari:** ni viwango vya mienendo sahihi ya kuzingatiwa katika uandishi/utangazaji wa habari. Wanataaluma wa tasnia ya habari hutumia maadili ya uanahabari kama dira ya kuwaongoza katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Mawazo mgando kuhusu jinsia:** Humaanisha kumwonyesha mtu wa jinsia moja au nyingine kwa namna ambayo inamtumia vibaya, kumbainisha kama kitu badala ya mtu na kumshushia hadhi.

**Uonyeshaji hasi wa jinsia:** Hili lipo katika lugha, mitazamo au uwasilishaji wa wazi-wazi au kuashiria, ambao una mwelekeo wa kuhusisha majukumu, tabia au mienendo fulani ya watu na jinsia zao kwa namna ambayo inawabana na kuwakwaza wahusika ndani ya jamii au sehemu tofauti-tofauti za jamii.

## UTEKELEZAJI WA SERA

*Sera ya Jinsia katika vyombo vya Habari* ndiyo itakuwa mwongozo wa mwenendo na utendaji kwa wamiliki wa vyombo vya habari, wachapishaji na wale wenye majukwaa ya kidijitali ambao ni wanachama wa Baraza la Habari Tanzania (MCT).

*'Sera ya Jinsia katika vyombo vya Habari'* inapaswa kusomwa sanjari na chapisho la 'Kanuni za Maadili kwa wanataaluma wa Habari' lililotolewa na Baraza la Habari Tanzania.

*'Sera ya Jinsia katika vyombo vya Habari'* ina lengo la kutengeneza mazingira salama na bora kwa ajili ya ufanyaji kazi ndani ya vyombo vya habari, kwa mfano:

i. Uwepo wa sera ambazo hazitoi mwanya wowote wa unyanyasaji wa kingono, na taratibu thabiti za kuripoti unyanyasaji;

ii. Mafunzo mahsusi yanayolenga kukabili changamoto za usalama wa wanawake ndani ya vyombo vya habari;

iii. Kujitahidi kukabili vizingiti vya kitamaduni ambavyo vinakwaza upatikanaji wa haki. Kwa mfano:

- Vituo vya habari vinavyohamishika; usafiri wa pamoja au kusindikiza wale wanaokwazika kwa kusafiri peke yao au kusafiri nyakati za usiku;
- Mafunzo mahsusi au 'Siku ya Wanawake'

vitengwe kwa lengo la kuwajengea wanawake hali ya kujiamini;

- Kuanzisha Dawati la Jinsia katika vyombo vya habari kuhakikisha wanawake wanashirikishwa katika misingi ya usawa;

iv. Kutoa habari ya ukweli juu ya mwanamke/mwanamme aliyefanyiwa ukatili au unyanyasaji wa kingono kwa kutafuta ushahidi kutoka kwenye vianzo visivyo na upendeleo na vya kuaminika;

v. Vyombo vya habari vitatoa kwa haki na usawa fursa kwa wanaume na wanawake katika kuandika na kutangaza habari;

vi. Wasimamizi wa redio na runinga wataongeza idadi ya vipindi vyenye mada mahsusi juu ya masuala ya jinsia—mada ambazo zitatoa changamoto dhidi mawazo mgando ya kijinsia; pia waandishi wa safu magazetini watafanya hivyo;

iv. Katika kuripoti masuala ya siasa, uchumi au vita, wanahabari watahakikisha sauti za wanawake zinasikika.

# A. SERA YA RASILIMALI WATU INAYOZINGATIA JINSIA NDANI YA VYOMBO VYA HABARI

Duniani kote, uhitaji wa rasilimali watu, wawe wanaume au wanawake, unazidi kushuka. Lakini kwa wastani, kuna idadi ndogo zaidi ya wanawake itakayobaki katika jumla ya rasilimali-watu inayohitajika. Sababu zilizoleta uwepo mdogo wa wanawake katika ajira ni za kimfumo na kitamaduni na uwepo wa idadi kubwa ya wanawake katika kazi za kibarua kuliko zile za ajira ya mkataba rasmi:

Aidha, wanawake huwa wanabaguliwa katika sekta mbalimbali na aina za kazi zilizopo na uhaba wa nafasi za kazi, hasa kwa wanawake vijana. Pana ubaguzi wa aina fulani wa watu ambapo wanawake, kama kundi, wanachukuliwa kama kundi ambalo ni duni kuliko kundi jingine—lile la wanaume! Iwapo sera za raslimali watu hazitatambua uwepo wa ubaguzi huu, hali hii hasi inayoumiza wanawake itaendelea.

## KUJALI USAWA WA KIJINSIA SEHEMU ZA KAZI

i. Waajiri katika vyombo vya habari—viongozi waandamizi, mameneja na mameneja wa raslimali watu wanahamasishwa kutilia maanani sera ya usawa wa kijinsia wakati wa kutoa ajira na katika uteuzi ili kuhakikisha kuna fursa sawa kwa wanawake katika ngazi zote za usimamizi na utaoaji uamuzi.

ii. Suala zima la mpango wa kubakiza waajiriwa mahali pa kazi na mipango ya siku za usoni inapaswa kutilia maanani wafanyakazi wa kike wenye uwezo;

iii. Vyombo vya habari vinahamasishwa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wao wananufaika na programu za mafunzo na ushauri ambao ni jumuishi kwa ajili ya wanawake na wanaume, lakini pakiwa na msisitizo zaidi kwa wanahabari wa kike;

iv. Vyombo vya habari vinapaswa kufuata sera ambazo zinapinga unyanyasaji wa kijinsia kwenye maeneo ya kazi, na

v. Vyombo vya habari vinapaswa viweke wazi utaratibu wa kukuza waajiriwa kikazi, kuwajengea uwezo, sera ya kuinua waajiriwa kwa haraka-haraka ambayo

inahakikisha wanawake na wanaume wana haki sawa katika kupata fursa ya kuwa waandishi wa habari mahususi.

## MWONGOZO JUU YA UNYANYASAJI WA KINGONO SEHEMU ZA KAZI

Mwongozo juu ya unyanyasaji wa kingono ni chombo cha kuangazia na kuondoa unyanyasaji sehemu ya kazi, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kingono na uonevu, mambo ambayo yamekuwa kero kubwa ulimwenguni kote. Utekelezaji wa Mwongozo huu utawezesha na uwepo wa sehemu za kazi ambazo hazina unyanyasaji wa kijinsia, sehemu ambazo waajiri na waajiriwa wanajali heshima, hadhi na faragha ya mtu na haki yake kudai usawa kazini.

## UNYANYASAJI SEHEMU ZA KAZI NI NINI?

Hii ni tabia ambayo inaathiri hadhi ya wanawake na wanaume, tabia ambayo inachukuliwa kama mwenendo ambao hautakiwi, usiokubalika, usiostahili, na ambao unaleta woga, uhasama, udhaifu au karaha katika mazingira ya kazi.

Ubaguzi usio wa jinsi ni ule ambao unahusisha, pamoja na mengine, haya yafuatayo:

- Uasilia, rangi au utaifa;
- Umri;
- Upungufu wa kimwili, kisomi, akili au afya ya akili;
- Ujauzito au uwezekano wa kuwa mjamzito;
- Hali ya kindoa au wajibu wa kifamilia na
- Dini

Baadhi ya unyanyasaji katika sehemu za kazi ambao umekithiri ni:

- Unyanyasaji wa kingono;
- Utongozaji wenye kero;
- Unyanyasaji wa maneno ambao huweza kuishia kwenye mtu kutishiwa, kufedheheshwa, kutusiwa;
- Picha zenye maudhi;
- Kutaka mfanyakazi kimapenzi;
- Kulazimisha au kutumia mabavu kufanya ngono na mtu, nk.

Iwapo hili au mojawapo ya haya linamfika mfanyakazi, tukio linapaswa kuripotiwa kwa msimamizi au Idara ya Rasilimali Watu.

## HATUA ZA KINIDHAMU

Tukio lolote la unyanyasaji litakapothibitishwa,

litatolewa uamuzi kwa mujibu wa taratibu na hatua za kinidhamu zilizowekwa. Baadhi ya hatua za kinidhamu zilizopo, pamoja na zingine zinazoweza kuchukuliwa, ni hizi:

- Ushauri;
- Onyo;
- Kusimamishwa kazi
- Kufukuzwa kazi

## B. KURIPOTI MASUALA YA KIJINSIA

Tafuta ukweli na kuuripoti kwa kina kadri iwezekanavyo

i. Wakati wote vyombo vya habari vitatumia njia za haki, zinazoaminika na zinazoeleweka kwa urahisi, katika kutafuta habari, picha na nyaraka juu ya watoto ambao wananyanyaswa kingono;

ii. Wanahabari wanahimizwa kuchunguza na kutafiti masuala ya jinsia ili waelewe mijadala inayoendelea kuhusu haki za kijinsia.

iii. Vyombo vya habari viwe na mipango ya mafunzo ambayo itaboresha weledi wa wanahabari wake juu ya masuala ya jinsia yaliyopo na yale yanayojitokeza katika sura mbalimbali.

iv. MCT itatumia mamlaka yake kama

chombo huru cha wanahabari cha kuihakiki tasnia ya habari kushirikiana na taasisi za mafunzo kuhakikisha kipengele cha jinsia kinakuwa ndani ya muhtasari wa vyuo vya uandishi wa habari.

## KUWA HURU KATIKA UTENDAJI

i. Vyombo vya habari vitakuwa vikichukua tahadhari badala ya kusubiri matukio kwa kutafuta maoni tofauti kutoka kwa wanawake na wanaume, bila kujali nafasi ya mtu katik jamii na;

ii. Wanahabari, kwa wakati wote, watajitahidi wasiwe na upendeleo na waepuke kujihusisha waziwazi na matamko au taasisi zenye malengo finyu ya kisiasa. Wanahabari waharakishe kusahihisha habari zozote za kupotosha juu ya wanawake/wanaume.

## USIEGEMEE UPANDE WOWOTE

i. Wanachama wa MCT wataongeza vipindi vinavyohusu masuala ya jinsia na kuruhusu wanawake zaidi kushiriki katika utayarishaji wa vipindi hivyo.

ii. Habari zinazohusu ukatili na unyanyasasaji wa kingono zinapaswa kuandikwa

na kupangiliwa kwa namna ambayo zitaeleweka kwa urahisi;

iii. MCT inatambua kwamba wanawake si kundi la watu wanaofanana kwa kila hali. Vyombo vya habari vitahamasishwa kuripoti habari-jumuishi za wanawake wote, habari ambazo hazikujikita kwenye tabaka za kijamii, hadhi ya mtu, na bila kujali kama wanaoripotiwa wanaishi vijijini au mijini. Hilo liwe ni pamoja na kupanua fursa kwa minajili ya wanahabari wa kike na wa kiume kutoa habari zihusuzo mada za aina zote, zikiwa ni pamoja na zile za masuala ya kijinsia.

`

## UWAJIBIKAJI

Wanahabari watawajibisha viongozi watunga sera kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa katika maeneo yao ya kazi kwa mujibu wa kanuni za kitaifa, kikanda na kimataifa ambazo Tanzania imezitilia sahihi au kuziridhia.

## MIZANIA NA KUTOPENDELEA

i. Thibitisha taarifa ulizopata kwa kusikiliza pande zote za habari unazotarajia kuchapisha au kutangaza, ukizingatia maslahi ya mwanamke;

ii. Hadhari na umakini uwepo katika kuripoti habari za ukatili wa kingono juu ya mwanamke iwapo tayari shauri la tukio-husika limeshafikishwa mahakamani. Hili ni muhimu ili kuepuka uwezekano wa kuharibu utaratibu mzima wa kisheria, na

iii. Habari zinazohusu unyanyasaji na ukatili wa kingono zisiandikwe kwa lugha ya jazba, kipropaganda au ya vijembe au kimafumbo.

## UNYANYAPAA NA UCHUNGU

Vyombo vya habari vitaepuka kuunga mkono chuki au kushadidia ukatili wa kijinsia. Vitapaswa kuepuka mambo yafuatayo:

i. Kutangaza au kuchapisha kwa kinagaubaga habari za ubakaji au ukatili wa kingono kwa namna ambayo itafanya waathirika watambulike;

ii. Kushadidia picha chafu na za ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

iii. Kuwadunisha wanawake kwa kuwabainisha kama viumbe dhalili wanaostahili kufanyiwa ukatili, labda tu pale ambapo ukatili ni sehemu ya habari inayosimuliwa;

iv. Kuwadunisha ama kuwatumia vibaya

wanawake kwa kuwaonyesha kama viumbe dhalili wasio na uwezo wa kufanya lolote mbele ya ukatili na unyanyasaji;

v. Kuwadunisha au kuwatumia vibaya wanawake na kuhujumu nafasi chanya waliyo nayo, na umuhimu wao katika jamii;

vi. Kushadidia unyanyasaji wa mawazo-mgando juu ya jinsia, na

vii. Kuchapisha habari ambazo zinaweza kuibua vurugu na chuki kutokana na uwasilishaji mbaya wa masuala ya jinsia au kutukuza ukatili dhidi ya wanawake.

## PUNGUZA MADHARA

Tasnia ya habari ina dhima ya kuripoti juu ya mambo yote na kwa usahihi kama iwezekanavyo. Hata hivyo, katika kutekeleza lengo hili, vyombo vya habari vitapaswa kuweka uwiano kati ya madhara na maumivu na mambo mbadala ambayo yangeweza pia kutimiza lengo la kuripoti ukweli. Mtangazaji hataripoti mambo ambayo, kulingana na muktadha, yanaonyesha tukio au matukio, yawe ya kuigiza au ya ukweli, kati ya haya yafuatayo:

i. Mtu ambaye, kwa mwonekano wake

ni mwenye umri wa chini ya miaka 18, akishiriki kwenye tendo la ngono au kujionyesha utupu;

ii. Vitendo vinavyoonyesha waziwazi tendo la ngono kwa njia ya kikatili;

iii. Ngono kati ya wanyama na binadamu, na

iv. Tendo la wazi la ngono linalomdhalilisha mtu na ambalo, kwa namna fulani, linashadidia chuki ya kijinsia na ambalo lina mwelekeo wa kuchochea chuki na kuleta madhara.

## LUGHA

i. Matumizi ya lugha inayoashiria ubaguzi au unyanyasaji wa kijinsia ni marufuku katika Vyombo vya Habari;

ii. Wanahabari watatambua heshima ya wanawake na wataepuka kutoa matamshi yenye mwelekeo wa kubagua watu kwa misingi ya kijinsia, na

iii. Wakati wa kuhariri na kuchambua usahihi wa taarifa iliyoletwa na mwandishi/ripota, kuandika vichwa vya habari au vidokezo muhimu vya habari na kuchagua picha za kutumia, vyombo vya habari viepuke kurahisisha mambo na kuripoti masuala ya kijinsia kwa njia potofu.

## MASOKO NA MATANGAZO

i. Vyombo vya habari vihakikishe kwamba viwango vya msingi vya uandishi wa habari vinatiliwa maanani katika matangazo ya biashara, na

ii. Fikra-mgando juu ya jinsia au uonyeshaji watu kwa namna ambayo inadhalilisha kijinsia usiruhusiwe katika matangazo.

## USALAMA

i. Kutenegeneza mazingira mazuri na salama kwa ajili ya mahojiano na mwathirika kwa kuwa na idadi ndogo ya wanaofanya mahojiano na wapigapicha na kamwe wasihusishwe watu wa nje;

ii. Badilisha jina na kuficha uso wa mtu ambaye amegunduliwa kuwa ni mwathirika wa ukatili au unyanyasaji wa kingono wakati wa kuripoti shauri-husika kwenye chombo cha habari, na

iii. Habari au picha ambazo zinaweza kuuweka hatarini usalama wa mwathirika (wa kike au wa kiume) zisiandikwe au kutangazwa.